# UTAKATIFU
## WA CHAGUZI ZA
# KIBAHÁ’I



*BARAZA LA KIROHO LA KITAIFA LA*
*WABAHÁ’I WA TANZANIA*

# UTAKATIFU
## WA CHAGUZI ZA
# KIBAHÁ’I



***BARAZA LA KIROHO LA KITAIFA LA WABAHÁ’I WA TANZANIA***

# MASWALI NA MAJIBU KUHUSU CHAGUZI ZA KIBAHÁ'I

*Baraza la Kiroho la Kitaifa*
*la Wabahá'i wa Tanzania*


***Kimehakikiwa na:***

*Kamati ya Uhakiki wa Tafsiri ya Kiswahili ya Kitaifa ya Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabahá'i wa Tanzania*

***Kimechapishwa na***

*Kamati ya Vitabu, Uchapishaji na Usambazaji ya Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabahá'i wa Tanzania*



*S.L.P. 585, Dar es Salaam, Tanzania.*
***Simu:*** *+255-685 637 422*

***Barua Pepe:*** *secretariat@bahai.or.tz*
*literature@bahai.or.tz*



***Toleo la: 2023***

**ISBN 978-9912-9985-1-3**



*© Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabaha'i wa Tanzania*

1. **Je, Tufanye nini ili tuwe imara na thabiti katika Agano?**

1. “Wajibu wa kwanza ulioamriwa na Mungu kwa watumishi Wake ni utambuzi wa Yule Ambaye ndiye Chimbuko la Ufunuo Wake na Chemchemi ya Sheria Zake, Ambaye huwakilisha Uungu katika vyote viwili; Ufalme wa Hoja Yake na ulimwengu wa muumbo. Yeyote atimizaye wajibu huu amefikia mema yote; na yeyote aliyenyimwa hilo amekengeuka, japokuwa awe mwanzilishi wa kila tendo jema. Inampasa kila mmoja afikiaye daraja hili adhimu kabisa, kilele hiki cha utukufu wa juu kabisa, kuzingatia kila agizo la Yule Ambaye ndiye Haja ya ulimwengu. Wajibu huu pacha hautenganishiki, wala mmoja haukubaliki bila ule mwingine. Hivyo ndivyo ambavyo imeagizwa na Yule Ambaye ndiye Chanzo cha uvuvio Mtakatifu.”

   *(Baha’u’lláh, Kitab-i-Aqdas, uk. 19, ki.1, Kiingereza)*

2. **Je, Chaguzi za Kibahá’i ni kati ya sheria za Kiroho? Je, ni muhimu kwa waumini kushiriki kwenye chaguzi?**

   2.“Bwana ameamuru kwamba katika kila mji, Nyumba ya Haki ianzishwe ambamo watakusanyika washauri kwa idadi ya Bahá... Inawabidi wawe walioaminiwa wa Yule Mwenye Rehema kati ya watu na wajione kama walinzi walioteuliwa wa Mungu kwa vyote viishivyo duniani.”

3. “Na sasa, kuhusu Nyumba ya Haki ambayo Mungu ameamuru kama chanzo cha mema yote na kuwekwa huru kutoka makossa yote, inapaswa kuchaguliwa kwa kura za wote, yaani, na waumini. Wajumbe wake wanapaswa wawe wadhihirishaji wa kicho cha Mungu na mapambazuko ya maarifa na uelewa, lazima wawe imara katika Imani ya Mungu na watakia mema wa wanadamu. Kwa Nyumba hii ina maana Nyumba ya Haki ya pili ianzishwe, na Nyumba za Haki hizi za pili zinapaswa kuchagua wajumbe wa Nyumba moja ya Ulimwengu.”
   *(Wasia na Agano la Abdu’l-Bahá, uk.4, Kiingereza)*

4. “Utaratibu wa Ulimwengu wa Baha’u’lláh ni mfumo ulioamriwa na Mungu ambao mataifa na watu wanautafuta sana. Ulianzishwa na Báb katika Bayán ya Kiajemi (kitabu Chake Kitakatifu), vipengele vya msingi wake vimeagizwa na Baha’u’lláh Mwenyewe, Utaratibu huu hauna kifani katika historia ya binadamu kwa kuwa kiwango chake cha haki na msimamo wake kwa ajili ya ufikiaji wa umoja wa binadamu kivitendo pamoja na uwezo wake wa kukuza mabadiliko na maendeleo ya ustaarabu wa ulimwengu. Hutoa njia ambayo kwayo Mapenzi ya Mungu huangazia njia za maendeleo ya binadamu na kuongoza hatma ya ujenzi wa Ufalme wa Mungu duniani.” *(Kutoka barua ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Wabahá’i wa Ulimwengu, 23 Machi 2007)*

5. “Kupitia muunganiko wa jitihada za kuendeleza mchakato wa uingiaji kwa makundi ushikao kasi kote duniani kupitia utekelezaji wa masharti ya Mpango wa Miaka Mitano, sasa ni muda muafaka kwa waumini kila mahali kujikita zaidi kwenye uimarishaji wa mchakato ambao kwa huo Mabaraza ya Kitaifa na ya mahali yanachaguliwa. Namna ya ushiriki wa wana-jumuiya watu wazima kwenye chaguzi hizi ni tabia bainifu ya Mfumo wa Baha’u’lláh; kwa kuwa ni wajibu ambao humpa upendeleo wa hali ya juu kila Mbahá’i kuchagua, kama raia mwenye wajibu kwa ulimwengu mpya unaoanzisha, muundo wa asasi zenye mamlaka juu ya utendaji kazi wa jumuiya ya Kibahá’i. Kuhusiana na suala hili, kutojali na kutotekeleza kwa upande wa muumini ni jambo geni kwa moyo wa Hoja. Marafiki wanapaswa wajitahidi bila kuacha kujiepusha na kutochafuliwa na tabia hizi haribifu, ambazo zimesababisha uharibifu wa uadilifu na mamlaka kwa asasi za utaratibu wa Ulimwengu unaoanguka.” *(Kutoka barua ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Wabaha’i wa Ulimwengu, 23 Machi 2007).*

**3. Je, nini kusudi la Utawala wa Kibahá’i; na je, unaweza kufananishwa na mfumo mwingine wowote?**

6. Ili kukuza maendeleo ya ustaarabu wa ulimwengu, Baha’u’lláh alibuni mfumo mpya wa kusimamia masuala ya kijamii ujulikanao kama Utaratibu wa Utawala wa Kibahá’i. Asasi zilizomo ndani ya utawala huu ni njia ambazo kupitia kwazo mwongozo na moyo wa Imani ya Baha’u’lláh hutiririka hadi kwa muumini binafsi.



7. “Itakuwa ni upotoshaji kabisa kulinganisha kati ya utaratibu huu wa kipekee, uliofikirika kitakatifu na mifumo yoyote mbalimbali ambayo akili za watu, katika nyakati tofauti tofauti za historia yao, zilibuni kwa serikali za mashirika ya kibinadamu. Kujaribu huku, kwenyewe kutafichua utovu wa utambuaji vyema wa ubora wa kazi ya mikono ya Mwanzilishi wake mkuu.” *(Shoghi Effendi, Utaratibu wa Ulimwengu wa Baha’u’lláh, uk.19, Kiingereza)*

*8*. “Ukuaji wa Mabaraza ya Kiroho ya Mahali ya Kibahá’i na ya Kitaifa katika wakati huu huhitaji hali mpya ya kifikra kwa upande wa wajumbe wake na pia kwa upande wa wale ambao huyachagua, kwa kuwa jumuiya ya Kibahá’i inajishughulisha katika mchakato mkuu mno wa kihistoria ambao unaingia katika hatua muhimu. Baha’u’lláh ameupa ulimwengu asasi za kufanya kazi katika utaratibu uliobuniwa kuelekeza nguvu za ustaarabu mpya.” *(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ujumbe wa Ridván, 1996)*

**4. Je, ni mazoea yapi yaepukwe kwenye chaguzi za Kibahá’i? Na je, kampeni na uteuzi vinaruhusiwa?**

9. “Kuhusu mazoea ya uteuzi kwenye chaguzi za Kibahá’i, hili Mlinzi anaamini kwa dhati kabisa kwamba kimsingi halipatani na moyo na umuhimu ambao ungepaswa kuhuisha na kuongoza chaguzi zote zifanywazo na Wabahá’i, ziwe za mahali au kitaifa. Kwa kweli, ni ukosefu wa mazoea haya ambayo huwa ndiyo kipengele kinachotofautisha na ubora uonekenao wa taratibu za uchaguzi wa Kibahá’i juu ya zile ambazo kwa kawaida zinahusishwa na vyama vya siasa na makundi. Hivyo, mazoea ya uteuzi yaliyo tofauti na moyo wa Utawala wa Kibahá’i, hayana budi kuachwa kabisa na marafiki wote. Kwa kuwa vinginevyo uhuru wa mpiga kura katika kuchagua wajumbe wa Baraza la Kibahái, utahatarishwa sana, na kuacha wazi njia kwa utawala wa nafsi za watu. Si hivyo tu, bali pia kitendo tu cha kuteua hatimaye husababisha uundwaji wa vyama—jambo ambalo ni geni kabisa kwa moyo wa Hoja.” *(Kutoka barua iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi, Miangaza ya Uongozi, uk.9, Na.32)*

10. “Aidha, mazoea ya uteuzi, yenye madhara mno kwa hali ya uchaguzi wa kimya kimya na wenye moyo wa ibada, huangaliwa kwa shaka kwa

kuwa hukipa haki kikundi cha walio wengi ambacho, chenyewe katika hali za wakati huu, mara nyingi huwa ni cha walio wachache kati ya wawakilishi wote waliochaguliwa, kunyima ile haki iliyotolewa na Mungu kwa kila mpiga kura kuwapigia kura wale tu ambao yeye kwa dhamira yake huamini ni wagombea wanaostahili kabisa.” *(Kanuni za Utawala wa Kibahá'i, uk. 64, Kiingereza)*

11. “Kwa kuongezea juu ya hatari hizi kubwa, mazoea ya uteuzi yana hitilafu kuu ya kuua ndani mwa muumini moyo wa ari, na wa kujiendeleza.” *(Kutoka barua iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini mmoja, Februari 1935)*

12. “Jihadharini, jihadharini, isije uvundo unukao wa vyama na watu wa nchi ngeni za magharibi, na njia zao ovu, kama ufanyaji njama, siasa za vyama na uenezaji wa habari—mazoea ambayo huchukiza hata kwa jina—daima yakaifikia jumuiya ya Kibahá'i, yakafanyiza ushawishi wowote ule juu ya marafiki, na hivyo kuharibu hali yoyote ile ya kiroho. Marafiki wanapaswa, kupitia moyo wao wa ibada, upendo, uaminifu na ukarimu, kukomesha mazoea haya maovu, na kutoyaiga. Ni hadi pale tu marafiki watakapoacha kuyajali kabisa na kujitakasa kutokana na maovu haya, ndipo roho wa Mungu atakapoweza kujipenyeza na kufanya kazi ndani ya jamii ya binadamu, na ndani ya jumuiya ya Kibahá'i.” *(Kutoka barua ya Mlinzi kwa marafiki huko Uajemi, 30 Januari, 1923: Tabia ya Kiroho ya Chaguzi za Kibahá'i, uk.1)*

**5. Je, jinsi gani waumini wajiandae kwa ajili ya chaguzi za Kibahá'i?**

13. “Jinsi ambavyo mpiga kura huitumia haki yake na upendeleo wa kupiga kura yake, hivyo ina umuhimu mkubwa. Maelekezo ya Shoghi Effendi katika kifungu hiki huelezea zaidi kuwa ‘kuweza kufanya chaguo la busara katika wakati wa uchaguzi, ni muhimu kwake kuwa karibu na kuendelea kuwa karibu na waumini wenzake, kujihusisha na shughuli zote za mahali, ziwe ufundishaji, utawala au zinginezo, na kwa moyo wote kushiriki kikamilifu katika mambo yote ya mahali pamoja na jumuiya za kitaifa na Mabaraza ya nchi yake. Ni kwa njia hii tu kwamba muumini anaweza kukuza ufahamu wa kweli wa kijamii na kujipatia hisia za kweli za uwajibikaji katika mambo yanayohusu maslahi ya Hoja. Maisha ya jumuiya ya Kibahá'i hivyo hufanya iwe wajibu kwa kila muumini mtiifu na mwaminifu kuwa mpiga kura mwenye akili timamu, aliyefahamishwa vyema na mwajibikaji, na pia humpa fursa ya kujiinua hadi daraja hilo’.” *(Kutoka barua ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Wabahá'i wa Ulimwengu, 23 Machi 2007)*

14. “Katika kuelezea chaguzi za Kibahá'i, Shoghi Effendi, kupitia barua iliyoandikwa kwa niaba yake, alisema kwamba ‘taratibu na mbinu za chaguzi za Kibahá'i zimekua, hakika, kwa ajili ya mojawapo ya madhumuni yake muhimu, ukuzaji katika kila muumini, wa moyo wa uwajibikaji. Kwa kutilia mkazo umuhimu wa kudumisha uhuru wake kamili katika chaguzi, humfanya iwe lazima kwake kuwa na juhudi na mshiriki aliyefahamishwa vyema katika jumuiya ya Kibaha'i aishimo’.” *(Kutoka barua ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Wabahá'i wa Ulimwengu, 23 Machi 2007)*

15. “Sharti tujizuie kutokana na kushawishi mawazo ya wengine, ya kumuombea kura mtu yeyote binafsi, lakini kutilia mkazo juu ya umuhimu wa kufahamishwa vyema zile sifa za ushirika zinazotajwa katika Nyaraka za Mpendwa wetu, na wa kujifunza zaidi kuhusu wenyewe kupitia tajiriba binafsi ya moja kwa moja badala ya taarifa na mawazo ya marafiki zetu”. *(Shoghi Effendi, Maelekezo ya Mlinzi, uk.23, Kiingereza)*

16. “Wakati inapaswa pasiwepo utajaji wa nafsi za watu kuhusiana na chaguzi za Kibahá'i, inafaa kabisa kwa waumini kujadili masharti na sifa za jumla katika asasi ya kuchaguliwa. Shoghi Effendi hutoa mwongozo ulio wazi kuhusu suala hili, “Nahisi kwamba utajaji wa nafsi za watu kabla ya uchaguzi ungeibua tofauti na kutoelewana. Kile ambacho marafiki wanatakiwa kufanya ni kufahamiana kikamilifu, kubadilishana mawazo, kujichanganya kwa uhuru na kujadili kati yao masharti na sifa hizo za jumla bila utajaji au uhusishaji, hata usio wa moja kwa moja jinsi gani, na watu binafsi.” *(Kutoka barua ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Wabahá'i wa Ulimwengu, 23 Machi 2007)*

**6. Je, Chaguzi za Kibahá'i zifanyike wapi? Je, mazingira na taratibu zipi zifuatwe siku ya uchaguzi?**

17. "Wachache waoneshe tahadhari kubwa mno ili chaguzi zifanywe kwa uhuru, kwa wote na kwa kura za siri. Aina yoyote ya njama, udanganyifu, hila na ulazimishaji sharti izuiwe na hairuhusiwi." *(Shoghi Effendi, Januari 1923, imetafsiriwa kutoka Kiajemi)*

18. "Kura ya mtu inapaswa iwe siri. Hairuhusuwi kutaja kwa vyovyote vile majina ya watu binafsi…" *(Shoghi Effendi, Januari 23, imetafsiriwa kutoka Kiajemi)*

19." Wakiitwa kuchagua katika uchaguzi wa Kibahá'i, waumini watambue kuwa wanafanya shughuli takatifu ya kipekee katika Mpango huu wa Mungu. Wanapaswa kuuendea wajibu huu katika hali ya sala, wakitafuta mwongozo na uthibitisho mtakatifu. Kama Shoghi Effendi alivyoshauri, "Wanapaswa kumgeukia kabisa Mungu, na kwa nia safi, uhuru wa kiroho na utakatifu wa moyo, washiriki kwenye uchaguzi". *(Kutoka barua ya Nyuumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Wabahá'i wa Ulimwengu 23 Machi 2007)*

20. "…Mpiga kura…huitwa kuchagua si yeyote isipokuwa wale ambao sala na tafakari zimemwongoza kuthibitisha." *(Shoghi Effendi, Kanuni za Utawala wa Kibahá'i, uk.66, Kiingereza)*

21. "Wapiga kura…wanapaswa, kwa sala na kwa moyo wa ibada na baada ya tafakari na kuwaza, wachague roho aminifu, nyoofu, zoefu na zenye uwezo na hodari ambazo hustahili ujumbe." *(Shoghi Effendi, Chaguzi za Kibahá'i, uk.317, Kiingereza)*

22. "Kwenye siku ya uchaguzi marafiki, kwa moyo wote wanapaswa washiriki katika chaguzi, kwa umoja na urafiki, wakigeuzia mioyo yao kwa Mungu, wakijitenga na vyote isipokuwa Yeye, na kutafuta uongozi Wake na kuomba msaada na Baraka Zake." *(Kutoka barua ya Mlezi kwa marafiki wa Uajemi, Februari 27 1923: Hali ya Kiroho ya Chaguzi za Kibahá'i, uk.1, Kiingereza)*



23. "…Wakati wa uchaguzi, marafiki wanapaswa kuwa katika hali ya sala, kutopendelea na kujitenga kutokana na nia za kiunia. Ndipo watakapoongozwa kuchagua wajumbe wanaofaa kwa ajili ya Mabaraza". *(Kutoka barua iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini mmoja, 7 Juni 1924)*

**Taratibu kuhusu kura za Wasiokuwepo:**

**24.** "Taratibu zile zile za upigaji kura zinapaswa kufuatwa, yaani, kura inapaswa kuwekwa na kufungwa ndani ya bahasha ya ndani isiyo na alama yoyote na bahasha hiyo iwekwe ndani ya bahasha nyingine kubwa ikiwa na jina la mpiga kura…" *(Kutoka barua ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya Kitaifa, 21 Januari, 1973)*

**7. Je, ni sifa zipi tuzizingatie wakati tunapowachagua wajumbe wa Mabaraza au wawakalishi wa Mkutano Mkuu wa Kitaifa?**

25. Wabahá'i wote wenye sifa njema na umri ulioruhusiwa wanastahili kupiga na kupigiwa kura katika chaguzi za Kibahá'i. Wale wenye umri kuanzia miaka 18 wanaruhusiwa kupiga kura lakini wao hawapigiwi kura. Wanaoruhusiwa kupigiwa kura ni wale wenye umri kuanzia miaka 21.

27. "Kati ya 'sifa muhimu' zilizotajwa na Mlinzi ni pamoja na zile za "uaminifu usiotiliwa shaka, moyo wa ibada usio na ubinafsi, akili iliyoelimika vyema, uwezo unaotambulika na tajiriba iliyokomaa". Kwa ufahamu ulioongezeka wa kazi za kutekelezwa na asasi ya kuchaguliwa, muumini anaweza kutathmini vyema wale ambao wanapigiwa kura. Kutoka miongoni mwa bwawa la wale ambao mpiga kura anaamini kuwa wanastahili kuhudumu, uchaguzi sharti ufanywe kwa uzingatiaji unaostahili wa vipengele vingine kama vile rika, anuwai na jinsia. Mpiga kura anapaswa kufanya chaguo lake baada ya kufikiria kwa makini kwa muda mrefu kabla ya uchaguzi wenyewe." *(Barua kutoka Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Wabahá'i wa Ulimwengu, 23 Machi, 2007)*

28. "Wapiga kura…wanapaswa, kwa sala na kwa moyo wa ibada na baada ya tafakari na kuwaza, wachague roho aminifu, nyoofu, zoefu na zenye uwezo na hodari ambazo hustahili ujumbe." (*Shoghi Effendi, Chaguzi za Kibahá'i, uk.317, Kiingereza)*

29. “Kuchaguliwa kwenye Baraza…siyo haki ambayo watu wana haki au heshima ambayo wangetamani kuipata, ni wajibu na dhima ambayo wao huweza kuitiwa. Madhumuni ni kwamba wale ambao huchaguliwa kwenye Baraza sharti wawe wanaostahili kabisa kwa ajili ya huduma hii.” *(Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, Utakatifu wa Chaguzi za Kibahá’i, uk.6, Na. 18, Kiingereza)*

30. “Muumini ana haki ya kujipigia kura mwenyewe wakati wa uchaguzi, kama kwa dhamira anahisi hamu kubwa kufanya hivyo. Hii siyo lazima imaanishe kwamba yeye ni mtaka makuu au mbinafsi. Kwa kuwa angeweza, kwa dhamira kuamini kwamba sifa zake humpa haki ya ujumbe katika asasi ya kiutawala ya Kibahá’i, na angeweza kuwa sawa. Jambo la muhimu, walakini, ni kwamba sharti awe mnyoofu katika Imani yake, na sharti atende kwa mujibu wa dhamira yake. Aidha, ujumbe katika Baraza au kamati ni aina ya huduma, na sharti isiangaliwe kama dalili ya ukuu wa kiasili au njia ya kujigamba.” *(Kutoka barua iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa Baraza la Kiroho la Kitaifa la India, Pakistani na Burma, 27 Machi 2998)*

**MIKUTANO YA MAHALI: UCHAGUZI WA WAWAKILISHI WA MKUTANO MKUU WA KITAIFA**

1. **Je, nani aliyepanga mfumo wa kuchagua wawakilishi na ufanyaji Mkutano Mkuu wa Kitaifa?**

31. “Imeandikwa dhahiri katika Maandiko ya Abdu’l-Bahá kwamba Mabaraza haya ya Kitaifa hayapaswi kuchaguliwa moja kwa moja na marafiki, hii inamaanisha kwamba, marafiki katika kila nchi wanapaswa kuchagua idadi fulani ya wawakilishi, ambao na wao watachagua kutoka miongoni mwa marafiki wote katika nchi wajumbe wa Baraza la Kiroho la Kitaifa…wapiga kura hawa wa pili ndipo, ama kupitia barua, au bora zaidi kwa kukusanyika pamoja, na kwanza wakishauriana juu ya masuala ya Hoja katika nchi yao nzima (kama wawakilishi kwenye Mkutano Mkuu), wachague kutoka miongoni mwa marafiki wote katika nchi hiyo wale tisa (9) ambao watakuwa wajumbe wa Baraza la Kiroho la Kitaifa.” *(Shoghi Effendi, Kanuni za Utawala wa Kibahá’i, uk.61, Kiingereza)*



**2. Je, nani huchagua wawakilishi?**

32. Kutokana na nukuu ya hapo juu, marafiki katika kila nchi wanapaswa kuchagua idadi fulani ya wawakilishi”. *(Shoghi Effendi, Kanuni za Utawala wa Kibahá’i, uk.61, Kiingereza)*

33. Idadi ya wawakilishi inayotengwa kwa kila nchi hutajwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kutokana na idadi ya Wabahá’i watu wazima waishio katika nchi yao. Baraza la Kiroho la Kitaifa ndipo hugawanya nchi katika eneo moja moja na kuamua idadi ya wawakilishi kwa kila eneo kutokana na idadi ya Wabahá’i watu wazima wa kila eneo husika. Maeneo haya, moja moja baadaye yanawajibika kuandaa mkutano wa eneo lao ambapo marafiki hujadiliana kuhusu masuala ya Imani na kuchagua idadi maalum iliyotajwa ya wawakilishi wa Mkutano Mkuu wa Kitaifa. Ni jukumu takatifu la waumini kushiriki katika mikutano hii ya maeneo ili kuhakikisha kuwa waumini wanaostahili kabisa wanachagualiwa kama wawakilishi wa Mkutano Mkuu wa Kitaifa.

**3. Je, mwakilishi lazima ahudhurie Mkutano Mkuu wa Kitaifa?**

34. “Ni lazima, hata hivyo, iwekwe wazi kwa kila mwakilishi aliyechaguliwa—ambaye daima lazima akumbushwe kwamba ni jukumu takatifu, na ikiwezekana kwa kweli ni bora ahudhurie mtu mwenyewe binafsi kwenye vikao vya Mkutano Mkuu, ajihusishe kwa bidii katika matukio yote, na awajulishe watendakazi-wenza wakati wa kurudi kwake, mafanikio, maamuzi na matarajio ya wawakilishi wa waumini waliokutana.” *(Shoghi Effendi, Kanuni za Utawala wa Kibahá’i, uk.65, Kiingereza)*

**4. Je, ni zipi Kazi mbili za Mwakilishi?**

36. “…wawakilishi wa waumini watambuliwao rasmi waliokusanyika sharti wasitumie tu haki muhimu na ya uwajibikaji ya kuchagua Baraza la Kitaifa, bali pia watimize kazi za asasi iliyotaalamika ya kushauriana na kushirikiana ambayo itasitawisha tajiriba, itaongeza heshima, itaunga mkono mamlaka, na kusaidia mashauriano ya Baraza la Kiroho la Kitaifa.” *(Shoghi Effendi, Kanuni za Utawala wa Kibahá’i, uk.62, Kiingereza)*

37. “Haitawezekana katika hatua hii kutojali umuhimu au kukadiria kupita kiasi maana ya kipekee ya asasi ya Baraa la Kiroho la Kitaifa—muhimili ambao shughuli za waumini katika…bara zima huangukia. Ni kuu mno nafasi yao, ni makubwa mno majukumu yao, ni za aina nyingi na ngumu kazi zao. Jinsi gani upendeleo ulivyo mkuu, jinsi gani ihitajivyo umakini kazi ya wawakilishi waliokusanyika ambao kazi yao ni kuchagua wawakilishi wa kitaifa ambao kwa kumbukumbu yao ya huduma hukuza hadhi na kusitawisha kumbukumbu za kihistoria za Hoja. *(Shoghi Effendi, Utawala wa Kibaha'i: Jumbe zilizochaguliwa 1922 – 19932, uk. 87-88)*



## CHAGUZI ZA MABARAZA YA KIROHO

1. **Je, Mabaraza ya Kiroho ya Mahali na ya Kitaifa ni asasi zilizoamriwa na Mungu?**

38. “Bwana ameamuru kwamba katika kila mji, Nyumba ya Haki ianzishwe ambamo watakusanyika washauri kwa idadi ya Bahá... Inawabidi wawe walioaminiwa wa Yule Mwenye Rehema kati ya watu na wajione kama walinzi walioteuliwa wa Mungu kwa vyote viishivyo duniani. Inawapasa washauriane pamoja na kufikiria maslahi ya watumishi wa Mungu, kwa ajili Yake, kama vile wafikiriavyo maslahi yao wenyewe, na wachague kile kinachostahili na kinachofaa. Hivyo ndivyo Bwana Mungu wenu alivyowaamuru. Jihadharini msije mkasahau kile ambacho kimefunuliwa dhahiri katika Waraka Wake. Mwogopeni Mungu, Enyi wenye kuona.” *(Baha'u'lláh, yamenukuliwa katika Kanuni za Utawala wa Kibahá'i, uk.38, Kiingereza)*

39. “Kuhusu uanzishwaji wa ‘Mabaraza ya Kitaifa’, ni jambo lenye umuhimu mkuu kwamba katika kila nchi ambapo hali huruhusu na idadi ya marafiki imekua na kufikia kiwango kinachofaa,…’Baraza la Kiroho la Kitaifa’ liundwe mara moja, mwakilishi wa marafiki katika nchi nzima.” *(Shoghi Effendi, Kanuni za Utawala wa Kibahá'i, uk.73, Kiingereza)*

40. “Baraza la Kiroho la Kitaifa, lililotajwa na Abdu'l-Bahá katika Wasia na Agano Lake kama ‘Nyumba ya pili ya Haki’, ni mamlaka kuu kabisa ya Utawala wa Kibahá'i katika kila nchi. Baraza la Kitaifa limeainishwa na Shoghi Effendi kama “mlinzi aliyeaminiwa na chanzo hasa cha shughuli za aina nyingi na maslahi ya kila jumuiya ya kitaifa katika ulimwengu wa Kibahá'i.” Yeye husema kwamba Mabaraza haya ‘hufanyiza asasi za uchaguzi kwa ajili ya uundaji wa Nyumba ya Haki ya Kimataifa, na yamepewa idhini ya kuongoza, kuunganisha, kuratibu na kuchochea shughuli za watu binafsi pamoja na Mabaraza ya Mahali yaliyomo ndani ya mipaka ya mamlaka yao.’” *(Mkutano Mkuu wa Kitaifa, taarifa iliyoandaliwa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, Desemba 1992)*

41. “Enyi mlio imara katika Agano: Abdu’l-Bahá hujishughulisha katika mawasiliano kamili na Baraza lolote la Kiroho ambalo limeanzishwa kupitia Baraka takatifu, na wajumbe ambao wamo katika hali ya ibada kabisa wakigeukia kwenye Ufalme Mtakatifu na ambao ni imara katika Agano. Yeye huambatana nao sana na ameunganishwa kwa mafundo ya milele. Hivyo mawasiliano nao ni ya dhati, ya daima na yasiyokatizwa.” *(Abdu’l-Bahá, yamenukuliwa katika Kanuni za Utawala wa Kibahá’i, uk.39, Kiingereza)*

**2. Je, kuna umuhimu gani wa kushiriki katika uchaguzi wa Baraza la Kiroho la Mahali?**

42. “Haya Mabaraza ya Kiroho ya Mahali yatatakiwa kuchaguliwa moja kwa moja na marafiki, na kila muumini aliyejitangaza ambaye amefikia umri wa miaka kumi na nane na zaidi, mbali na kujitenga na kujitwalia mwelekeo wa kutojali na ulio huru, sharti alione kama jukumu lake takatifu kushiriki kwa dhamira na kwa uangalifu, katika uchaguzi, ‘uimarishaji na ufanyaji kazi wenye ufanisi wa Baraza Lake la Mahali.’” *(Shoghi Effendi)*

43. “Hebu tukumbuke ahadi Yake (ya Abdu’l-Bahá) dhahiri na aliyoirudia mara kwa mara kwamba kila Baraza lililochaguliwa katika hali ya kutakasika, ya utovu wa ubinafsi na ya kujitenga, kwa kweli, limeteuliwa na Mungu, kwamba maamuzi yake kwa kweli huongozwa, kwamba wote sharti wajisalimishe kikamilifu na kwa furaha kwenye maamuzi yake.” *(Shoghi Effendi, Kanuni za Utawala wa Kibahá’i, uk.65-66, Kiingereza)*

**3. Je, ni lipi kusudi la kufanya chaguzi za kila mwaka?**

44. “Kwa kuwa kama Abdu’l-Bahá alivyorudia kusisitiza kwamba Mabaraza ya Kibahá’i yapo chini ya uongozi na ulinzi wa Mungu. Chaguzi, hasa ziwapo za kila mwaka, huzipa jumuiya nafasi nzuri ya kurekebisha kasoro au mapungufu yoyote ambayo Baraza linaweza kuwa nayo kutokana na vitendo vya wajumbe wake. Hivyo njia salama imeanzishwa ambayo kwayo aina ya ujumbe ndani ya Mabaraza ya Kibahá’i inaweza kuendelea kuinuliwa na kuboreshwa. Hata hivyo, kama ilivyoelezwa hapo awali, asasi ya Baraza la Kiroho kwa namna yoyote ile isifananishwe na, au kukadiriwa tu kupitia sifa binafsi za wajumbe wanaoliunda.” *(Kutoka barua iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi kwa muumini mmoja, 15 Novemba, 1935)*



**4. Je, ni baadhi ya mambo gani ya kuzingatiwa kwa makini katika kuchagua Baraza la Kiroho la Mahali au la Kitaifa?**

45. “Shoghi Effendi huona kuwa mahali popote ambapo idadi ya waumini watu wazima imefikia tisa (9), Baraza la Mahali lazima liundwe. Yeye huona kwamba hili ni suala la lazima kuliko kuwa kama kitendo cha hiari kabisa…” *(Barua iliyoandikwa na katibu wa Shoghi Effendi kwa niaba yake)*

46. “Hakuna akidi ihitajikayo katika ufanyaji wa uchaguzi wa Baraza la Kiroho la Mahali. Kanuni hii pia inahusika katika suala la chaguzi ndogo. Jambo tu la ukweli kwamba chini ya watu tisa huchagua wajumbe wa Baraza la Kiroho la Mahali halibatilishi uchaguzi…Kama mjuavyo, Baraza la Kitaifa linaweza daima kuangalia hali zinazozunguka uchaguzi wa Baraza la Kiroho la Mahali na kutumia busara zao kuamua kama, kwa kuzingatia hali zote, uwepo wa Baraza la Kiroho la Mahali utambuliwe.” *(Kutoka barua ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa Baraza la Kiroho la Kitaifa la Equedor, 16 Aprili, 1996)*

47. “Kuhusu swali ulilouliza kama katika chaguzi za Mabaraza ya Kiroho wapiga kura sharti wapige kura za idadi kamili ya kura tisa au wanaweza kupiga kura chini ya idadi hii. Kwa kuwa ujumbe wa Baraza la Kiroho, kwa mujibu wa kanuni za Utawala wa Kibahá’i, umewekewa ukomo wa wajumbe tisa kwa wakati huu, hufuatia kwamba hakuna kura ya uchaguzi inayoweza kufaa isipopigwa kwa idadi hiyo kamili. Kwa hiyo, ni wajibu mtakatifu kwa kila Mbahá’i mpiga kura kupiga kura tisa, siyo zaidi wala siyo pungufu…ili kuhakikisha kwamba matokeo ya chaguzi za Baraza la Kiroho yatafaa na juu ya msingi mpana wa uwakilishi kadiri iwezekanavyo.” *(Kutoka barua ya Machi 27, 1940 iliyoandikwa kwa niaba ya Mlinzi kwa Baraza la Kiroho la Kitaifa la Visiwa vya Uingereza)*

**5. Je, upi uwe mtazamo wetu kwa matokeo ya chaguzi za Baraza?**

48. “Mara tu chaguzi za Baraza zinapomalizika, matokeo lazima kwa dhamira na bila shaka yakubaliwe na jumuiya nzima ya waumini, si lazima kwa sababu yanawakilisha sauti ya ukweli au mapenzi ya Baha’u’lláh, bali kwa kusudi kuu la kudumisha umoja na maelewano katika jumuiya. Aidha, kukubali kura ya wengi ni njia pekee inayofaa na ya kivitendo ya kumaliza mivutano kwenye chaguzi. Hakuna ufumbuzi wowote kwa kweli unaowezekana.” *(Kutoka barua iliyoandikwa kwa niaba ya Mlinzi kwa muumini mmoja, 10 Julai, 1939)*



**UUNDAJI WA HALMASHAURI ZA KIBAHÁ’I ZA KANDA**

1. **Je, zipi zilikuwa sababu za kuanzishwa kwa Halmashauri za Kibahá’i za Kanda?**

49. “Upanukaji wa jumuiya ya Kibahá’i na utata uongezekao wa masuala yanayoyakabili Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa katika nchi kadhaa umeileta Hoja kwenye hatua mpya katika maendeleo yake. Umetufanya sisi katika miaka ya hivi karibuni tuchunguze vipengele mbalimbali vya usawa kati ya mfumo wa ukatikati na wa ugatuaji madaraka. Katika nchi chache tumeidhinisha Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa kuanzisha Halmashauri za Kibahá’i za Kanda au Kamati za Ufundishaji na za Kiutawala za Maeneo. Kutokana na tajiriba iliyopatikana katika utendaji wa asasi hizi, na kutokana na uchunguzi wa kina wa kanuni zilizoelezewa na Shoghi Effendi, tumefikia uamuzi kwamba sasa ni muda muafaka kwetu kurasimisha msingi mpya wa utawala wa Kibahá’i kati ya ngazi za mahali na za kitaifa, zilizo na asasi za aina maalum, zitajwe kama ‘Halmashauri za Kibahá’i za Kanda.” *(Kutoka barua ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu) kwa Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa, 30 Mei, 1997)*

**2. Je, jinsi gani Halmashauri za Kibahá’i za Kanda zinavyoundwa katika nchi yetu kwa wakati huu?**

50. Nchi yetu ni mojawapo ya nchi ambazo zimetajwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kuanzisha Halmashauri zake za Kibahá’i za Kanda kwa uteuzi. Hivyo, mwongozo ufuatao ulitolewa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwenye kiambatanisho cha barua ya 30 Mei 1997, iliyokuwa na kichwa cha habari ‘Uundaji wa Halmashauri za Kibahá’i za Kanda katika Nchi Kadhaa, Sifa na Kazi zao’.

51. “Imeachwa juu ya Baraza la Kiroho la Kitaifa kuamua ikiwa idadi ya wajumbe iwe tano, saba au tisa.

52. “Upigaji kura hufanyika miongoni mwa wajumbe wa Mabaraza ya Kiroho ya Mahali katika eneo, unaofanana na ule wa uchaguzi wa Halmashauri za Kibahá’i za Kanda, walakini matokeo ya uchaguzi hufanya orodha ya siri ya mapendekezo kwa ajili ya Baraza la Kiroho la Kitaifa, ambalo huteua wajumbe wa Halmashauri kutoka wateuliwa

hawa na wengine, wakiwemo watu waliopendekezwa na wajumbe wa Halmashauri za Usaidizi ambao ndani ya mipaka ya maeneo yao ya mamlaka eneo hilo limo.”

**Yamekusanywa 2012.**

**Masahihisho: 2023**